

**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA
MAFUNZO YA UFUNDI STADI**



TAARIFA KWA UMMA

**MATOKEO YA UHAKIKI WA WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KATIKA
MKUPUO WA MACHI 2024/2025**

Baraza linataarifu umma kuwa matokeo ya uhakiki wa waombaji waliochaguliwa kujiunga na masomo kwa mkupuo wa Machi, 2024/2025 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada yametoka rasmi leo tarehe **15 Machi, 2024**.

Jumla ya waombaji **9,353** kati yao Wanawake walikuwa 4,979 (53.2%) na Wanaume 4,374 (46.8%) waliwasilishwa kwa ajili ya uhakiki kutoka katika vyo viliyokidhi vigezo vya kudahili katika mkupuo huu. Kati yao, waombaji **9,121 (Wanawake 4,867 na Wanaume 4,254)**, sawa na asilimia **97.5** walikuwa na sifa za kujiunga na programu walizoomba, na waombaji **232 (2.5%)** hawakuwa na sifa katika programu walizoomba.

Waombaji wote walioomba kujiunga katika program mbalimbali wanaweza kupata taarifa zao za uhakiki kwa kutumia misimbo iliyotumwa kwenye namba zao za simu kwa bonyeza kitufe *“Uhakiki mkupuo wa Machi, 2024/2025”* katika tovuti ya Baraza www.nactvet.go.tz. Baraza linawasisitiza waombaji wote kutunza misimbo watakatyotumiwa kwani ndio itatumika katika udahili mara wafikapo chuoni.

Baraza linavielekeza vyo kuwasajili wanafunzi wenye sifa na watakaowasili vyo kwa ajili ya kuanza masomo kuanzia tarehe **25 Machi, 2024**; na kwa kutumia misimbo itakayotumwa na Baraza kwenye namba za waombaji. Chuo kitakachokiuka taratibu za udahili, hatua stahiki dhidi ya chuo husika zitachukuliwa.

Aidha, vyo vimepewa nafasi ya kurekebisha na kuwasilisha taarifa za waombaji ambazo hazikuwa sahihi kuanzia leo tarehe 15 hadi 17 Machi, 2024.

**IMETOLEWA NA: KATIBU MTENDAJI
(NACTVET)
15 MACHI, 2024**